TANGAZO LA SERIKALI NA. 114 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA KAGONGWA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Kagongwa ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama.

________

JEDWALI

________

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira –nukta 472790.27MS, 9573620.36KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS84$^{O}$35'38.28"MA kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 475641.14MS, 9573396.33KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS4$^{O}$15'38.48.55"MG kwa umbali wa kilomita 3.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 455348.84MS, 9570154.15 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ84$^{O}$32'09.57" MG kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira – nukta 472503.03MS, 9570384.08KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ4$^{O}$15'42.99"MS kwa umbali wa kilomita 3.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A hadi ulipoanzia".

Dodoma,
6 February, 2023.

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na*
*Maendeleo ya Makazi*